


COVID-19 na Jinsia

Mwongozo wa vijana balehe na vijana wadogo

Katika kipindi hiki cha mashaka, tunatakiwa kutambua kuwa ni jinsi gani COVID-19 inatuathiri tofauti kulingana na jinsia zetu.



Jinsia ni nini?



Sisi sote - wanawake, wanaume, wasichana na wavulana -wanashawishiwa na majukumu ya jinsia na matarajio. Inaathiri jinsi

tuanvyofikiria na tabia zetu, tunavaa nini na tunanguvu kiasi gani ya kufanya maamuzi. Wanawake wanatarajiwa kufanya kazi za nyumbani bila malipo na kuwatumza watoto, wakati wanaume wanachukuliwa kuwa wanaoandalia familia mahitaji, kupata pesa kwa ajili ya familia. Lakini majukumu haya yanaweza kubadilika.

Kwanini tuahitaji kujua kuhusu jinsia na COVID-19

1. Wanawake na wasichana wanafanya kazi nyingi za malezi bila malipo.




Wanawake na wasichana wadogo wengi wanafanya kazi Zaidi bila malipo katika kipindi hiki cha kizuizi kutokana na COVID-19. Hii ni pamoja na kuwatumza wagonjwa, kutoa huduma ya ziada ya matunzo yawatoto, upishi, kuosha vyombo na nguo pamoja na kazi ya shule na kujitunza. Hii ni pamoja na kuwatumza watu wagojwa, kufanya kazi zaidi ya malezi kwa mtoto, kupika, kuosha vyombo na kufua nguo na bado kazi ya shule na kujitunza wenyewe.



Tunahitaji kuwa makini kwa jinsi tunavyojisikia na wengine pia. Tunahitaji kujitunza sisi wenyewe na wengine na kuungana na wengine.

2. Upatikaji wa huduma ya afya ya uzazi na ujinsia ni mdogo.



Katika kipindi hiki, inaweza kuwa vigumu kupata huduma za uzazi wa mpango, condom na huduma ya afya ya mama na mtoto. Hii inaweza kusababisha ujauzito usiyopangwa, utoaji mimba usio salama, matatizo katika ujauzito na kujifungua, na magonjwa ya ngono, pamoja na VVU.

3. Ukatili wa kijinsia unaongezeka.



Nyumbani sio sehemu salama kwa kila mtu. Kwa baadhi ya nchi, tunaona ongozoko la ukatili wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na ukatili wa majumbani. Mtu yeyote anaweza kukumbana na ukatili, lakini wanawake, watoto na makundi maalumu wako kwenye hatari zaidi.

4. Wanaume wengi wanaungua sana.



Ushahidi unaonyesha kwamba wanaume wanaathirika Zaidi kwa COVID-19 kuliko wanawake. Tunajua pia kwamba wanaume na wavulana kwa ujumla hujiweka zaidi kwenye hatari katika maisha yao kama njia ya kuonyesha uanaume wao. Wao hutafuta huduma za afya mara chache kuliko wanawake na wasichana kama vile kwenda hospitali wakati wakiwa wanaumwa sana au kutokutumia dawa zao.



Kwa habari zaidi tembelea:

WHO - www.who.int/emergencies/diseases/novel-coronavirus-2019

UNAIDS - www.unaids.org/en/covid19




Hatua tunazoweza kuchukuwa sisi sote ambazo itasaidia kila mtu

Huduma zisizo lipiwa



Wanume vijana na wawulana wanaweza na wanapaswa **kupika, kusafisha na kufanya** na kwenda kununua vitu.



Wanaume vijana na wawulana wanaweza na wanapaswa **kuwatumia wadogo zao, ndugu zao wazee na wanafamilia wagojwa.**



Kumbuka!

Wamama wadogo na wasichana ndio wanaofanya sana hii kazi. Lakini hii huathiri elimu yao na inamaanisha wana muda kidogo wa ziada.



Afya ya uzazi na ujinsia na haki



Wakati wote pata idhini kutoka kwa mwenzi wako kufanya ngono, hata ikiwa uko katika mahusiano. Ikiwa mwenzi wako hataki kufanya

kufanya ngono, au anakubali kufanya ngono na kisha anabadili mawazo yake (kwa mfano, kwa sababu hauna kondomu), lazima uheshimu uamuzi wao.



Jadili na mfanye uamuzi wa pamoja kuhusu kufanya ngono salama kutumia kondomu na/au njia za uzazi wa mpango.

Epuka ngono isiyo salama kwa sababu inaweza kuwa vigumu kupata matibabu ya VVU / Magonjwa ya ngono, huduma ya afya ya mama na mtoto au huduma za utoaji mimba salama.



Kumbuka!

Ngono bila idhini ni ukatili wa kingono.



Jifunze Zaidi kuhusu idhini kwenye <https://frontlineaids.org/resources/sexual-and-reproductive-health-information-for-young-people/>

Pata taarifa kwa waelimisha rika wanaoamika, wahudumu wa afya na vyombo uhakika. Tembelea: UNFPA - www.unfpa.org/covid19



Kumbuka!

Ikiwa unahisi wasi wasi, sonona/huzuni au kuchanganyikiwa, zungumza na mtu au piga simu kwa mhudumu wa msaada wa kisaikolojia na kijamii aliye karibu na wewe.

Kukabiliana na ukatili



Ikiwa wewe au mtu yeyote katika nyumba yako yuko katika **hatari** kubwa, piga simu polisi au huduma za dharura.



Wasiliana na **marafiki, familia na majirani**. Pata msaada kwa mtu unayemuamini.



Ikiwa una wasiwasi kuhusu **ukatili wa majumbani**, wasiliana na namba za msaada au mtandao wa ushauri.



Kuwa mtulivu, zungumza mambo na jiondoe kwenye mgogoro ambao unaweza geuka na kuweza kuwa ukatili. Kunywa pombe kupita kiasi kunaweza kufanya hali iwe mbaya zaidi.

Aina za ukatili



Ukatili wa kimwili
Mfano kugogwa, kupigwa kupigwa kofi, tabia ya kutishia kutishiwa



Ukatili wa kihisia
Kama vile kupaza sauti, kuonewa, kukosolewa, kudhibiti, mhemko wa kihisia usiotarajiwa



Ukatili ya kingono
Mfano kubaka, kulazimisha ngono kugusa kusiko stahili au kudhalilisha.



Kumbuka!

Ukatili wa kihisia pia ni aina ya ukatili wa majumbani.

